

TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA SOKO LA AFRIKA SANA.

Mradi wa Soko la Afrika Sana, Upo katika Kata ya Kijitonyama. Lengo kuu la kujenga mradi huu ni kukuza na kuimarisha biashara kwa kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo kuingia katika mfumo rasmi wa Biashara, kuongeza ajira na kuweka mazingira bora kwa wateja wanaotegemea soko hili kupata huduma mbalimbali

Gharama za mradi huu wa Soko umefikia kiasi cha **shilingi 140,053,238.00**, kwa kujenga nguzo, paa na vizimba **40**.

Kabla ya ujenzi huu. Soko hili lilikuwa na nafasi kwa ajili ya wafanyabiashara **37**, ambao walikuwa wanafanya Biashara zao katika mazingira duni na yasiyo na mvuto kwa kibiashara.

Kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma za soko katika eneo hili, Manispaa iliamua kuvunja vibanda vilivyokuwepo na kujenga jengo hili ambalo lina nafasi 80 za Biashara na mazingira bora na salama kwa wafanyabiashara, wateja na watumiaji wengine.

Ujenzi wa Mradi huu umeleta manufaa ya kiuchumi kwa makundi mbalimbali kama ifutavyo:

- Nafasi za Biashara zimeongezeka kutoa **37** mpaka **80** na hivyo kupunguza biashara holela mitaani kwa kuongeza biashara ambazo ni rasmi.
- Mazingira ya soko yamekuwa yakuvutia salama na mazuri kwa wafanyabiashara, wateja na watumiaji wengine.
- Ongezeko la mzunguko wa Biashara utaongeza uchumi wa wafanyabiashara na mapato ya Manispaa.

MRADI WA UJENZI WA SOKO AFRICASANA KIJITONYAMA



VIZIMBA VYA MRADI WA SOKO LA AFRICASANA KIJITONYAMA

